

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA KUMI NA TATU**

**19 APRILI, 2018**



## **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

### **MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA KUMI NA TATU – TAREHE 19 APRILI, 2018**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

### **III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

### **IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

#### **OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

#### **104. MHESHIMIWA KASUKU SAMSON BILAGO (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Kaya zinazonufaika na Mfuko wa TASAF kwa vigezo vya umaskini baada ya kukidhi vigezo zimeanza kupata wakati mgumu na usumbufu mkubwa ikiwa mmoja wa wanakaya ni kiongozi wa Serikali ya Kijiji. Mfano baba wa kaya ndiye anakidhi vigezo vya kunufaika na mafao ya TASAF huku mama akiwa Mjumbe wa Serikali ya Kijiji, matokeo yake anaondolewa kuwa mnufaika na kuamuliwa kurudisha fedha yote aliyokwishanufaika nayo:-

- (a) Je, kuwa Mjumbe wa Kijiji kunaondoa umaskini wa Kaya;
- (b) Je, Kaya maskini inapataje uwezo wa kurudisha fedha walizotumia;

(c) Je, ni kwa nini Serikali isianganalie upya vigezo vya Wanufaika wa TASAF kwa kushirikisha wadau wengi.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**105. MHESHIMIWA HAWA ABDULRAHMAN GHASIA (MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati mifereji ya maji na matuta ambayo yalijengwa zaidi ya miaka 50 iliyopita katika Mji wa Mikindani ili kupunguza athari ya maji ya bahari kwenye Mitaa na Makazi ya Watu hasa kipindi cha mvua kali.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**106. MHESHIMIWA HASSAN ELIAS MASALA (NACHINGWEA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni nini kauli ya Serikali katika kushughulikia tatizo la migogoro ya mipaka katika Kambi za JKT

Nachingwea na Kikosi Namba 41 Majimaji na Vijiji vinavyozunguka Kambi hizo.

## **WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

### **107. MHESHIMIWA ALLY SALEH ALLY (MALINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Tanzania inaonekana kupanua uwanda wake wa kidiplomasia kwa kuanzisha Balozi mpya maeneo kadhaa; lakini pia kumekuwa na malalamiko ya makazi ya Wanabalozi wa nchi hii huko ughaibuni:-

- (a) Je, Serikali haioni haja ya kuwekeza katika eneo hili kwa kujenga ofisi ambazo pia zinaweza kuwa kibiashara;
- (b) Kama hilo linafanyika; je, limefanyika wapi na wapi hadi sasa.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **108. MHESHIMIWA ANDREW JOHN CHENGE (BARIADI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Katika miaka ya 80 Wananchi wa Vijiji vya Mwanchumu, Salaliya na Matongo

walitoa maeneo yao kwa Serikali ili yatumike kwa shughuli za kilimo zilizokusudiwa kufanywa na Gereza la Matongo. Lakini kwa sasa maeneo hayo hayatumiki na Magereza kikamilifu:-


Je, Serikali ipo tayari kurejesha maeneo hayo ambayo hayatumiki kikamilifu kwa Wananchi wa Vijiji hivyo.

**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**DODOMA  
19 APRILI, 2018**



**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**